**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga

*Dkt. Jackson Ndung'u Mwangi, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha KCA, S.L.P. 56808-00200, Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-8791-4846; Barua pepe ya mawasiliano: jigmwas@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*14 Novemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Dhana ya Vijana, Kitumbua Kimeingia Mchanga, Uhalisia.*

**IKISIRI**

Katika ulimwengu wa sasa, kuna mabadiliko chungu nzima yanayoshuhudiwa duniani yanasababishwa na masuala anuwai kama vile maendeleo ya kiteknolojia pamoja na utandarithi yanayoathiri pakubwa maisha ya vijana. Nchini Kenya, vijana wana umuhimu wa kipekee kwani wanatekeleza majukumu muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi. Isitoshe, idadi ya vijana kote ulimwenguni imeendelea kuongezeka kila uchao na imepiku ile ya wazee. Kwa hivyo, ni nyema kujadili changamoto zinazowakabili na kupendekeza hatua za kukabiliana nazo. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua changamoto zinazowakumba vijana pamoja na athari zake katika ya tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga ya S.A Mohamed (2000). Mada hii ilichaguliwa kwa misingi kwamba vijana wanakumbwa na changamoto nyingi katika maisha yao zinazowaathiri kwa kiasi cha haja na kutinga juhudi za kuafikia jaala zao. Utafiti huu ulilenga kubainisha changamoto zinazowakumba vijana katika tamthilia hii na kutambua mbinu ambazo vijana hawa wanazua ili kukabiliana nazo. Nadharia ya Uhalisia ilitumika kwa sababu ilionekana kufaa zaidi kuchanganua changamoto zinazowakumba vijana. Hii ni kwa sababu changamoto hizi zina uhalisia mkubwa katika maisha yao. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza na kueleza namna changamoto za vijana zinavyojitokeza katika tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga na kisha kubainisha hatua zinazochukuliwa kuzitatua changamoto hizo. Utafiti huu ni wa kimaelezo na kiudhamano kwani ulihusisha kuchanganua matini zinazohusiana na mada husika. Sampuli katika utafiti huu iliteuliwa kimakusudi kwani ndiyo ingempa mtafiti data aliyonuia kuipata. Ni bayana kuwa utafiti huu utaifaa jamii ya wasomi wanaoshughulikia maswala ibuka katika jamii.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

**APA CITATION**

Mwangi, J. N. (2022). Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 69-77. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959.

**CHICAGO CITATION**

Mwangi, Jackson Ndung'u. 2022. "Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 69-77. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959.

**HARVARD CITATION**

Mwangi, J. N. (2022) "Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 69-77. doi: 10.37284/jammk.5.2.959.

**IEEE CITATION**

J. N. Mwangi, "Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 69-77, Nov. 2022.

**MLA CITATION**

Mwangi, Jackson Ndung'u. "Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Nov. 2022, pp. 69-77, doi:10.37284/jammk.5.2.959.

## UTANGULIZI

Utafiti huu ulidhamiria kuangazia changamoto zinazowakumba vijana katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* iliyoandikwa na S. A. Mohamed (2000) na kutambua mbinu zinazotumiwa kukabiliana na changamoto zenyewe. Kulingana na ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu vijana ya 2014-2017, vijana ni watu wa jinsia zote mbili ambao umri wao ni baina ya miaka kumi na mitano hadi ishirini na minne. Kundi hili linaweza kupanuliwa hadi miaka thelathini na mitano kutegemea muktadha halisi na sera za maendeleo ya vijana kimaeneo na kitaifa.

Sera ya kitaifa kuhusu vijana nchini Kenya inamweleza kijana kama mtu yeyote ambaye umri wake ni baina ya miaka kumi na mitano na thelathini, kutokana na tarakimu za Wizara ya Vijana na Michezo iliyobuniwa mwaka 2008. Kufuatia maelezo haya pamoja na matokeo ya sensa ya 2009, asilimia sabini ya watu wote nchini Kenya ni vijana. Kulingana na ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu vijana, dunia ina vijana bilioni moja, asilimia themanini na watano wakiwa katika mataifa yanayoendelea. Ripoti hii inaeleza vijana kuwa katika msukumo wa mabadiliko na wana sauti yenye nguvu kuhusu haki zao na jinsi ya kukabili na kutatua changamoto zinazowakumba. Baadhi ya vijana wana dhana mpya kuhusu maisha na wamekuwa mstari wa mbele katika kuonyesha suluhisho kwa changamoto za kimaendeleo na kujenga daraja baina ya jamii na tamaduni tofauti.

Mabadiliko katika jamii ni hakika na jinsi jamii inavyobadilika, ndivyo vijana wanavyobadilisha majukumu yao. Mfumo wa zamani wa maisha umebadilika na hivyo kuyabadilisha majukumu ya vijana. Maisha ya kiasili ya Mwafrika yalihusu jamii nzima na watoto walikuwa mali ya jamii nzima. Katika hali hii majukumu ya kila mtu yalikuwa bayana. Vijana wa kiume walifunzwa majukumu na wazazi wa kiume, wale wa kike wakiandamana na wazazi wa kike ili kufunzwa majukumu yao. Vijana walikwenda shuleni nao wazazi wakiwa katika shughuli za kutafuta ajira na riziki. Nyingi ya asasi zilizowawekea misingi vijana zimeporomoka na kuwaacha vijana bila mwelekeo maalumu wa kuwafunza mambo muhimu katika maisha. Vijana wameelezewa kama viongozi wa kesho na tegemeo la jamii ya kesho. Msingi wa vijana ukiyumbayumba nalo taifa litakosa mwelekeo.

Chepkwony (2005) anaeleza ujana kama kipindi kilichojaa uhai kati ya utoto na utu uzima. Kulingana na Chepkwony, kundi la vijana lina umuhimu mkubwa katika jamii yoyote ile. Katika jamii zote, watu wazima wanategemea vijana kuendeleza kizazi cha kesho. Watu wazima kwa hivyo wana mshawasha wa kupitisha kwa kizazi cha vijana amali na utamaduni wa jamii. Kufuatia haya, kuna shinikizo kubwa kwa vijana katika harakati za kujaribu kuwafanya wakubali na kufuata vigezo na mahitaji ya jamii hasa wakati sehemu kubwa kati yao inaelekea kutokubaliana na matakwa haya.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

Nafasi ya vijana katika uandishi imeangaziwa na waandishi wengi wa hivi karibuni kama vile Walibora katika *Siku Njema* (2000) na *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Momanyi - *Tumaini* (2008) pamoja na tamthilia kama vile *Kifo Kisimani* (2001) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004) za Kithaka wa Mberia. Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ni mfano mzuri wa tamthilia inayoangazia changamoto zinazowakumba vijana katika jamii na athari zake katika maisha yao. Baadhi ya changamoto zinazowakumba vijana zinahusiana na malezi, kuchaguliwa wake, kuchaguliwa taaluma, anasa, utabaka na hata matumizi ya dawa za kulevya.

Ingawa vijana ni sehemu kubwa ya idadi ya watu nchini Kenya na katika ulimwengu, wanaonekana kukumbwa na changamoto nyingi zinazotokana na visababishi tofauti. Changamoto zinazowakumba vijana zimeangaziwa na waandishi pamoja na vyombo vya habari. Baadhi ya changamoto hizi zinahusiana na malezi, matumizi ya dawa za kulevya, mahusiano ya kijamii, elimu, kupuuzwa na kufanyiwa uamuzi, kukosa nafasi za uongozi, tamaduni za kigeni na teknolojia. Kutokana na hali hii utafiti huu unalenga kutathmini changamoto za vijana katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* na kubainisha mbinu wanazotumia vijana hawa katika kusuluhisha matatizo wanayokumbana nayo katika jamii.

Kuna waandishi wengi ambao wameshughulikia suala la matatizo yanayowakumba vijana katika jamii. Mutua (2007), alitafiti kuhusu mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Anaonyesha kuwa wazee na vijana kwa jumla wana hisia mseto kwa kuwa wanaunga mkono na pia kupinga ukombozi wa mwanamke. Alidokeza pia kuwa wanawake wanapata shida nyingi wanapojaribu kujikomboa na kutafuta haki kutoka kwa dhuluma za mwanamume. Maoni ya Mutua yataufaa utafiti huu sana kwani yanaonyesha matatizo ambayo wanawake kwa ujumla wanayapitia.

Obure (2012), ameshughulikia dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya mbili, *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006). Katika utafiti wake, alijikita katika wahusika wa kike pekee. Utafiti wake ulichangia katika kuangazia changamoto zinazowakumba vijana wanawake. Utafiti wetu unahusu vijana kwa jumla wa kike na wa kiume. Utafiti wake ulimsaidia mtafiti kuzimulika changamoto za wahusika wa kike. Isitoshe, Naliaka (2012), alihakiki hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Katika kazi yake, ameangazia changamoto zinazowakumba vijana katika jamii kama vile matumizi ya dawa za kulevya, ufisadi, ukosefu wa malezi bora, ukosefu wa ajira na umaskini. Baadhi ya changamoto hizi zinafanana na zile zilizoangaziwa katika utafiti huu. Kwa hivyo, maoni yake yatakuwa mchango mkubwa katika utafiti huu.

## MSINGI WA NADHARIA

Mada yetu inayohusu uchunguzi wa changamoto zinazowakumba vijana katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* iliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii inaafikiana na yale tuliyoyashughulikia katika mada yetu. Uhalisia ni tapo la kifasihi ambapo kazi za fasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Kazi hizi za fasihi zinasawiri hali halisi ya maisha katika jamii husika. Misingi ya uhalisia iliwekwa na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake Austhetik (1820-1829). Katika kazi yake Hegel, alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi ya kifasihi ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda kulingana na jinsi alivyochochewa na hali iliyomo. Chanzo cha nadharia ya uhalisia kilikuwa ni maeneo ya Ulaya katika karne ya kumi na tisa ambapo mapinduzi ya viwanda yalizusha mambo mapya kama vile kuzuka kwa miji, umaskini na matatizo ya maisha yaliyotokana na upanuzi wa miji hiyo. Shida hizi ziliwafanya wanasiasa na waandishi kuanza kukejeli na kupuuza ulimbwende uliokuwa ukithaminiwa enzi hizo na watunzi ambao matamanio yao yalikuwa ni ya kijonzi tu yakilinganishwa na shida zilizowakabili watu katika mazingira yao.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), uhalisia kama tapo la kuwaelekeza watunzi ulianza kudhihirika mwaka wa 1800 nyakati za mwandishi wa Kifaransa Flaubert (1850). Lukacs (1963), mfuasi wa Karl Marx kutoka Hungary ni mmoja wa wataalamu wanaohusishwa na nadharia hii. Aliamini uhalisia ulifaa kusawiriwa katika ukamilifu wake na vilevile picha ya uhalisia inayoshughulikiwa ni lazima ichunguzwe kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

undani ili kuzieleza sheria za mabadiliko ambazo husababisha uhalisia kwa wakati fulani. Wanauhalisia wanaamini kuwa yale yanayoshughulikiwa katika maandishi fulani ni lazima yaweze kuthibitika katika ulimwengu halisi.

Kwa muhtasari, ifuatayo ndiyo mihimili ya nadharia ya uhalisia:

- Kazi za fasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Kazi hizi zinasawiri hali halisi ya maisha katika jamii husika.
- Wahusika au mhusika hutenda kulingana na jinsi anavyochochewa na hali ya kisaikolojia aliyomo.
- Uhalisia unatoa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahsusi.
- Ukweli unapatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za binadamu akiwa katika mazingira yake halisi ya kijamii. Mazingira ni lazima yasawiriwe yalivyo bila kutiliwa chumvi.
- Kila kizazi kina uhalisia wake. Uhalisia katika kizazi kimoja unaweza kuwa tofauti katika kizazi kingine.

Kwa mujibu wa utafiti huu, tuliongozwa na nguzo zote tano za nadharia hii katika kuchanganua changamoto zinazowakumba vijana na mbinu wanazozua katika kukabiliana na changamoto zinazowaandama maishani katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*.

## NJIA ZA UTAFITI

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia njia ya kusoma na kuchanganua vitabu mbalimbali. Alisoma na kuhakiki tamthilia ya Kiswahili iitwayo *Kitumbua Kimeingia Mchanga* iliyoandikwa na S. A. Mohamed (2000) ambayo ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Uhakiki huu hasa ulijikita katika masuala ya vijana. Pia, mtafiti alirejelea vitabu mbalimbali kwa minajili ya kufafanua hoja zake. Kamusi mbalimbali zilitumika pamoja na makala tofautitofauti yanayozungumzia changamoto za vijana. Mtafiti alisoma makala mbalimbali kwenye mtandao kuhusu changamoto za vijana na sehemu ya nadharia. Pia, alisoma tamthilia zingine zinazohusiana na mada husika ili kulikuza swali la utafiti.

Isitoshe, alisoma kazi mbalimbali ambazo zimeandikwa kuhusu Nadharia ya Uhalisia kwa lengo la kuielewa zaidi kwa kuwa ni nguzo kuu katika kuchanganua changamoto zinazowakumba vijana. Vilevile, alizingatia maoni ya wataalamu wa fasihi ili kufaulisha utafiti wa mada yake.

Hatimaye, data aliyoikusanya aliichanganua kulingana na lengo la utafiti pamoja na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia. Utafiti huu kwa kiwango kikubwa ulikuwa wa maktabani.

## CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA

### Utangulizi

Katika utafiti huu tunashughulikia changamoto zinazowakumba vijana katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Kimani na Njogu na Chimerah (1999:28) wanaeleza kuwa chanzo cha msanii katika uandishi wake ni jamii fulani finyu. Hali zilizoikumba jamii hiyo hupewa muktadha pana ili kuigubika jamii pana. Ili kusawiri mambo yanayoiathiri jamii, sehemu hii itachanganua changamoto wanazokumbana nazo vijana katika jamii kama vile malezi, utabaka, anasa, uavyaji mimba, kuchaguliwa mchumba na matumizi ya dawa za kulevya.

### Changamoto Katika Malezi

Kwa mujibu wa tamthilia hii ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, vijana wanakumbwa na changamoto nyingi mno katika malezi kutokana na mabadiliko anuwai yanayodhihirika katika jamii husika. Katika ukurasa wa 9, Bi. Tukaije anakili waziwazi kuwa suala la kuwalea watoto wao, linakabiliwa na changamoto zisizo na kifani. Anadai kuwa kuwalea watoto hususan wa jinsia ya kike ni kazi ngumu sana kwani wasichana wanawindwa na wanaume kila uchao. Anadokeza kuwa wasichana wanaohadaika na kuingia kwenye mtego wa windo hili, huishia kukiharibu kitumbua chao, kupata mimba na hata wengine huishia kuiavya mimba ile.

> ***BI. TUKAIJE****:…toka umezaa mayai, hata ukayalalia, hata yakatotoa vifaranga, hata*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

> *ukavilisha vifaranga na kivitazama vinakua, na jicho lako juu mbinguni ukivilinda na paka…..na watoto wa siku hizi walivyo bibi'ngu* (uk. 9).

Dondo hili linadhihirisha kuwa kwa kweli, suala la kulea watoto ni tata na changamano kwani siku hizi watoto wanakulia katika mazingira yaliyojaa uchafu, hadaa na mabadiliko mengi kutokana na mwingiliano wa tamaduni za kigeni. Kwa hivyo, ni jukumu la kila mzazi kuchukua hatua ya kuwalinda na kuwaonya watoto wake ipasavyo.

Katika ukurasa wa 11, Bi. Tukaije anaendelea kubainisha jinsi ulezi wa watoto ulivyozingirwa na matatizo chungu nzima. Anadai kuwa vijana wa siku hizi wanalelewa katika mazingira machafu mno yaliyojaa dawa za kulevya, fujo na uasherati mwingi. Anadai kuwa licha ya yeye na sahibu wake Bi. Sikitu kutoka kwenye aila zinayojiweza kifedha na kiuchumi, mali si suluhisho la matatizo yanayowakumba vijana kwani mazingira ya kuwalea watoto yamejaa uchafu usio kuwa na kifani.

> ***BI. TUKAIJE:*** *…Pesa tunazo Alhamdulilahi, lakini haiwezekani kuishi kwa fedha tu. Pesa si kila kitu. Ina mwanzo na kikomo chake. Makinda tuliyonayo yanakuwa katika mazingira mabaya: fujo, uchafu na huu unga ulioingia. Sasa hizo ndizo mbolea za watoto wetu kukulia…* (uk. 11).

**Anasa**

Anasa ni hali ya kuzipenda raha nyingi za kimwili kama vile ngono ya kiholela, umalaya, densi, ulevi pamoja na tafrija. Anasa ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazovuruga maisha ya vijana. Katika kuiweka wazi changamoto hii, mtunzi wa tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia mchanga* amesawiri baadhi ya wahusika kama wapenda anasa na walionaswa katika mtego wa mitindo ya maisha waliyoiiga bila kuielewa vizuri. Mwandishi anawachora vijana kama wapenda anasa.

Kwa mujibu wa tamthilia hii, inabainika waziwazi kwa vijana wengine, hususan wa jinsia wa kike wamejitosa katika lindi la anasa, tabia ambayo inahatarisha maisha yao. Bi. Tukaije anahofia kuwa ndoa wanayoitarajia kati wa binti yake Maua inaweza kukosa kujibu kwani Maua amejiingiza katika anasa za kila aina na kuhatarisha maisha yake. Bi. Tukaije anadai kuwa Maua si maua tena kwani ameeneza harufu yake mtaani kote, hana subira na hatulii kamwe. Inadaiwa kuwa Maua ameibuka na tabia ya kutembea na vijana mtaani kiholela bila ya kujali na kuzingatia tamaduni za jamii yake.

> ***BI. TUKAIJE:*** *…anayeolewa ni huyu Maua asiye na subira. Anayepita kueneza rangi na harufu yake mitaani...* (uk. 13).

Hidaya mpenziye Fikirini anadaiwa kuwa amejiingiza katika anasa kwani kila uchao, yeye anaonekana akiwa amezingirwa na wanaume na hakosi kwenye densi. Kwa mujibu wa Bi. Haja, Hidaya si hidaya tena na hajatosha kuwa mke kwani kila uchao anashiriki katika anasa huku akiandamana na vijana wanaodaiwa kuwa na sifa mbaya kijijini. Bi. Haja anadokeza kuwa amemwona Hidaya mara nyingi akiwa mitaani huku akipepesuka na kuyumbayumba kwa ajili ya kunywa pombe. Isitoshe, inadaiwa kuwa Hidaya pamoja na vijana wengine huenda kushiriki katika densi na pia hujihusisha na shughuli ya ufuska. Haya yanadokezwa katika ukurasa wa 27.

> ***BI. HAJA****: …si mara moja wala mbili nimeshamuona katiwa katikati ya wanaume... wakiyumba na kupepesuka na kucheka… mpaka hivi juzi akicheza, naye, sijui chanuko, sijui foliti… kigori mzima. Hadhara ya watu, tena mchana si usiku…* (uk. 27).

Mifano hii inadhihirisha waziwazi kuwa vijana wanajihusisha na suala la anasa kupita kiasi, jambo linalowaathiri wao wenyewe na kuleta mtafaruku miongoni mwa wazazi wao. Kwa mujibu wa tamaduni za jamii ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, nafasi ya msichana ni kutulia nyumbani na kungojea mume ambaye angeteuliwa na wazazi wake. Kwa hivyo, Maua na Hidaya walikuwa wamesha uasi utamaduni wao na kuiga mienendo ya kigeni.

**Uavyaji Mimba**

Katika jamii ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, vijana hususani wa jinsia ya kike wanadaiwa kujihusisha na shughuli ya uavyaji mimba ambayo kwa kawaida inadhuru afya yao na kuleta kero kwa wazazi wao na jamii kwa ujumla. Bi. Mwatima

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

anadai kuwa vijana wa siku hizi wanashiriki ufuska na wanapopata mimba, wao huishia kuiavya na kuendelea na tabia zao za anasa. Bi. Mwatima anadai kuwa ana idhibati kuwa Hidaya na wasichana wengine wa kijiji chao wamejihusisha na shughuli potovu ya uavyaji mimba kama inavyodhihirika katika ukurasa wa 20.

> ***BI. MWATIMA:*** *Hashakum! Watoto watu wazima, nasikia hivi majuzi ameharibu…hayo mambo ya siku hizi ya kutoa pesa uvyazwe mzigo uliokulemea* (uk. 20).

Kulingana na Bi. Mwatima, ni wazi kuwa watu wa siku hizi wakiwemo vijana wameibuka na mtindo wa kuavya mimba baada ya kujihusisha na mapenzi kiholela.

Isitoshe, Bi. Tukaije anamweleza Bi. Sikitu kuwa watoto wa siku hizi wanalelewa katika mazingira yaliyojaa uovu na uchafu mwingi. Anadai kuwa mtoto wa kike hana amani kwani anawindwa kila uchao na wanaume waliojaa hadaa na wanapotimiza uchu wao na kuwatinga wasichana mimba, wanapendekeza uavyaji mimba ili wasitambulike. Haya yanabainika katika ukurasa wa 11.

## Kuozwa kwa Lazima

Suala la wasichana kuozwa kwa lazima lina uhalisia mkubwa katika baadhi ya jamii za Kiafrika. Vyombo vya habari vimechangia pakubwa kuangazia changamoto hii ambapo jamii imeshuhudia wasichana wadogo wakiachishwa shule na kuozwa bila hiari yao wenyewe. Ni dhahiri kwamba katika baadhi ya jamii za Kiafrika, mwanamke anapobaleghe huwa amefikisha umri wa kuolewa na hutafutiwa mume na kuingizwa katika ndoa bila hisia zake mwenyewe kutiliwa maanani.

Katika jamii hii inayosawiriwa na tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, imebainika kuwa vijana hawana nafasi kamwe ya kujichagulia wapenzi wao ila wanachaguliwa na wazazi wao. Bi. Haja (Mamake Bw. Mambo) anaonekana kutekeleza wajibu wa kipekee kuhakikisha kuwa Fikirini hafungi ndoa na Hidaya ambaye ni kipenzi chake na aliyejichagulia mwenyewe. Katika ukurasa wa 33, inadhihirika kuwa Bw. Mambo ameshamchagua Subira kuwa mke wa Fikirini na kusisitiza kuwa kamwe hataki Fikirini aoane na Hidaya, msichana aliyejichagulia mwenyewe. Isitoshe, Bi. Tukaije anafurahi sana anapopatana na Bi. Sikitu kwani anaelewa fika kuwa Subira ataolewa na Fikirini ambaye ametoka kwenye familia inayojiweza kifedha.

Katika ufukweni mwa bahari, Bw. Nia anakili kwamba tamaduni za jamii zao zilizoenziwa tangu jadi na babu zao za kuwachagulia wanao wachumba zimepitwa na wakati na katika dunia ya sasa, hazina nafasi. Anadai kuwa ni nyema vijana wa siku hizi wapatiwe uhuru wa kujichagulia wachumba kwani nyakati na hali za maisha zimebadilika na ulimwengu unaenda kwa kasi mithili ya upepo uvumao baharini. Bw. Nia anadai kuwa ni vyema kupiga msasa baadhi ya tamaduni zinazoendelezwa na jamii husussan katika taasisi ya ndoa kwani nyingi yazo ni dhalimu.

## Utabaka

Utabaka ni hali ya jamii kugawika katika makundi mbalimbali kulingana na uwezo wao wa kiuchumi. Tabaka ni kundi la watu linaloundwa na watu wenye sifa sawa za kiuchumi. Umaskini ni hali ya kukosa mali, ni ufukara au uhitaji. Ubepari husababisha matabaka kwa kuwa ni wachache tu wanaomiliki rasilmali. Mfumo wa Ubepari ambao huthamini pesa sana huwafanya wasio na pesa kutaabika.

Katika jamii ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, suala la utabaka linadhihirika sana na lina athari ya kipekee katika sekta mbalimbali za jamii hii ikiwemo taasisi ya ndoa. Bi. Haja hataki Fikirini aoane na Hidaya kwa sababu Hidaya ni mtoto wa tabaka la chini, anaishi katika Madongoporomoka (makazi ya wachochole na walalahoi) na familia yake ni ya kimaskini. Inatambulika kuwa Bi. Haja anataka Fikirini afunge ndoa na Subira, kwani ametoka kwenye familia inayojiweza kifedha. Bw. Mambo anaonekana kuafikiana na mawazo ya Bi. Haja na kudai kuwa, ndege wa aila moja, huburuka kwa pamoja kama inavyodokezwa katika uk. wa 26.

> ***BW. MAMBO:*** *…Lakini, hebu twambie Bi. Mkubwa: mbali ya kwamba Hidaya ni mtoto wa kimaskini, na ukoo wake hauna mashiko mazuri* … (uk 26).

Suala hili linadhihirisha kuwa utabaka umekita mizizi katika jamii hii na walio na uwezo wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

kiuchumi huungana na kuoana ili kuendeleza hali zao za kibepari.

Bi. Mwatima ambaye ametoka katika familia inayojiweza na ambaye ni rafiki wa aila ya Bw. Mambo anadhihirisha wazi kuwa utabaka umejikita katika jamii. Na yeye anataka tu kujihusisha na familia zenye uwezo wa kifedha kama Bi. Mwatima anaendeleza kasumba za kukuza utabaka pale anapowarai, Bw. Mambo na Bi. Sikitu wazue mbinu zozote zile kumzuia Fikirini kuoana na Hidaya kwani ni msichana aliyetoka katika familia ya ufukara, anaishi katika maeneo ya kimaskini na wazazi wake hawana chochote ila ni wachochole tu.

> ***BI. MWATIMA:*** *…Lo! Vitoto vinaanza mambo vingali vikambaa. Maskini mama yake…huyu wa Bi. Tiba Madongoporomoka…*

**Kuchaguliwa Taaluma**

Katika jamii hii, vijana hawana uhuru wa kujichagulia taaluma wanazozipenda ila wazazi wao wanajitahidi kwa hali na mali kuwachagulia. Katika ukurasa wa 15 hadi 18, Bw. Mambo anaonekana kukereka anaposikia Faki na Fikirini wakichambua na kuhakiki kitabu cha fasihi kilichoandikwa na Mwandishi Zanga. Anadai kuwa fasihi si taaluma bora ya vijana kusomea kwani inawavuruga vichwa, inawaduwaza na haina kipato cha haja. Baada ya kukamilisha mawasiliano katika simu yaliyodhihirisha jinsi anavyojihusisha na biashara za magendo, anawakemea wawili hawa na kuwaambia kuwa wakitaka kufaulu katika Maisha, ni sharti wajihusishe na taaluma zinazohusiana na biashara. Anahitimisha kwa kusema kuwa ulimwenguni kuna taaluma mbili kuu na muhimu ambazo wanapaswa kujihusisha nazo ambazo ni biashara na sayansi ya uongozi ila si upuuzi wa hadithi zinazopatikana katika vitabu vya fasihi.

> ***BW. MAMBO:*** *Haya ndiyo mambo ninayotaka mzungumzie na msomee: Biashara, biashara, kazi aliyoifanya ntume mwenyewe, haimtupi mtu… si upuuzi wa hadithi zenu… mkikosa kusomea biashara msomee sayansi ya uongozi…* (uk. 18).

**Dawa za Kulevya**

Katika Jamii ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, vijana wanakumbwa na changamoto za kutumia dawa za kulevya. Katika ukurasa wa 18, Bw. Mambo anapowasiliana kwa simu, inabainika kuwa yeye na wengine ni washiriki wa ulanguzi wa dawa za kulevya.

> ***BW. MAMBO:*** *...Aha, mambo mazuri? Lini itafika dawa? Thamani yake? Majumba kumi ya ghorofa?* (uk. 18).

Ni muhimu kutambua kuwa wanaoendeleza ulanguzi wa dawa za kulevya huwa wanalenga kuwauzia vijana na kuwaacha wakiangamia huku wakikumbwa na changamoto chungu nzima.

Isitoshe, matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana ndiyo husababisha matatizo anuwai maisha mwao kama vile kujiunga na magenge ya uhalifu na mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

Isitoshe, Bi. Tukaije anapomtembelea Bi. Sikitu analalamika kuwa vijana wa siku hizi wanakulia katika mazingira mabovu yaliyojaa uchafu chungu nzima ukiwemo matumizi ya dawa za kulevya kama inavyojitokeza katika ukurasa wa 11.

> ***BI. TUKAIJE:*** *…makinda tuliyonayo yanakua katika mazingira mabaya: fujo, uchafu na huu unga ulioingia. Sasa hizi ndizo mbolea watoto wetu za kukulia…*

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kuwa vijana wanaathiriwa na mazingira yaliyojaa dawa za kulevya zinazowaathiri kila uchao.

## MBINU ZINAZOTUMIWA NA VIJANA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBWA

Licha ya kuwa vijana wengi wanakumbana na changamoto chungu nzima katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, wanaibuka na mbinu anuwai za kukabiliana na matatizo wanayokumbana nayo.

Kwanza kabisa, Fikirini anaushikilia msimamo wake wa kumuoa Hidaya na kukataa kata kata shinikizo la Baba yake la kupendekeza aachane na Hidaya na kumuoa Subira. Kutokana na msimamo dhabiti aliokuwa nao Fikirini, mwishowe kabisa Bw. Mambo analegeza msimamo wake na kuamua kufuata uamuzi wa Fikirini japo shingo upande. Isitoshe, Fikirini anadhihirisha ukakamavu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

kutokana na jinsi anavyojaribu kumshawishi babake kuitikia uamuzi wake kama inavyodokezwa katika ukurasa wa 32.

> ***FIKIRINI:*** *…kuchagua ni kama kutia mkono kizani: ni bahati nasibu! Na si kwamba ving'aavyo vyote ni dhahabu…* (uk 32).

Kwa hivyo, vijana wanazua mbinu za kipekee na kukabiliana na wakubwa wao ili kusuluhisha matatizo yanayowakumba.

Pili, Bi. Sikitu anazinduka na kuamua kumrai mumewe kuitikia chaguo la Fikirini la kuoana na Hidaya. Katika kufanikisha hili, Bi. Sikitu anaamua kumshawishi mumewe azinduke na kumwacha mwanawe ajifanyie uamuzi kuhusu suala hili tata la ndoa. Anamwomba amsikize mwanawe na ampe uhuru wa kujichagulia mchumba wake kama inavyodokezwa katika ukurasa wa 47. Isitoshe, Bi. Sikitu anamrai bwanake aache taasubi ya kiume na utabaka kwani hamsikizi yeye kwa vile ni mwanamke na anamdharau Bw. Nia kwa sababu ni mvuvi na anaishi katika maisha ya umaskini.

> ***BI. SIKITU:*** *Humsikilizi Fikirini kwa kuwa ni mtoto uliyemzaa. Humsikilizi Bw. Nia kwa kuwa ni muuza samaki. Hunisikilizi mimi kwa kuwa mwanamke…lazima nihisi unanidharau…* (uk 46).

Isitoshe, Bw. Mambo anapoendelea kushikilia msimamo wake mkali, Bi. Sikitu anatishia kuondoka na kurudi kwao nyumbani, jambo linalomfanya Bw. Mambo kubadili nia yake na kumwitikia Fikirini kuendelea na mipango yake ya kumuoa Hidaya. Ni bayana kuwa ili kukabiliana na changamoto zinazowakumba vijana, ni nyema wazazi waweze kubadili nia zao, wawaelewe watoto wao na waweze kuzinduka. Isitoshe, ni nyema wazazi waweze kuwasikiliza watoto wao na kuwapa uhuru wa kujiamulia baadhi ya masuala yanayoathiri maisha yao.

vilevile, ni nyema wazee waweze kuzinduka na kufutilia mbali tamaduni kandamizi zinazowadhulumu vijana. Licha ya kuwa Bwana Nia ametoka kwenye tabaka la chini na anajihusisha na biashara duni ya kuvua samaki ili aweze kujikimu kimaisha, yeye amezinduka na anaelewa fika kuwa majira na nyakati zimebadilika. Anakua mstari wa mbele kuzielewa shida zinazowakumba vijana na kuamua kwenda kuzungumza na kumrai Bw. Mambo aache kumdhulumu Fikirini na ampe uhuru wa kujiamulia hatima yake kuhusu ndoa. Katika ukurasa wa 46, inabainika kuwa Bw. Nia alichukua jukumu la kuzungumza na Bw. Mambo lakini akakataa kumsikiza kwa sababu yeye ni wa tabaka la chini na anajishughulisha na biashara duni. Isitoshe, Bi. Sikitu ni mwanamke aliyezinduka na yuko tayari kutatua changamoto zinazowakumba vijana. Anamrai mumewe ampe mwanawe Fikirini uhuru wa kujichagulia mke, jambo ambalo analiitikia baadaye.

Suala la nne ambalo linajaribu kutatua matatizo yanayowakumba vijana ni kuwa serikali inabuni na kuzua mikakati kabambe ya kuwashika na kuwahukumu walanguzi wa dawa za kulevya. Katika ukurasa wa 65, Bw. Mambo anakamatwa na Inspekta Juma kwa tuhuma za kujihusisha na ulanguzi wa dawa za kulevya. Suala la Bw. Mambo kujihusisha na ulanguzi wa dawa za kulevya linadhihirika alipokuwa akizungumza na simu ukurasa wa 18. Anadai kuwa dhamani ya dawa za kulevya walizoziagiza kutoka nchi ya nje zina dhamani ya majumba kumi ya ghorofa. Isitoshe, pia inspekta wa polisi (Inspekta Juma) pia anadaiwa kuwa mlanguzi wa dawa za kulevya. Bw. Mambo anadhihirisha haya kutoka anaposhikwa na Inspekta yuyu huyu.

> ***INSPEKTA:*** *Unatuhumiwa kuwa mfanyi biashara wa magendo wa dawa za kulevya…*
>
> ***BW. MAMBO:*** *Hata wewe inspekta Juma? Aah, Haya wataingia waliyomo na wasiomo lakini…*

Nukuu hii inabainisha kuwa ulanguzi wa dawa za kulevya ni suala tata mno katika jamii kwa kuwa lina athari mbaya sana kwa vijana. Jambo nzuri ni kwamba serikali inachukua jukumu la kukabiliana na walanguzi hawa.

## HITIMISHO

Kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika kuwa vijana hukumbana na matatizo chungu nzima wakiwa katika azimio la kuyatimiza malengo yao. Baadhi ya matatizo ambayo vijana wanakumbana nayo katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ni kama vile, tatizo katika malezi, uavyaji mimba, anasa, utabaka na matumizi ya dawa za kulevya.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.959

Imedhihirika pia kuwa, licha ya vijana kukumbana na matatizo anuwai, wao wanaibuka na mbinu mbalimbali za kuyatatua matatizo hayo kama vile vijana kubuni mikakati kabambe ya kukabiliana na wakuu wao wanaowadhulumu. Pia, kuna wazee wanaozinduka na kuwasaidia vijana katika kukabiliana na matatizo yao kwa mfano Bw. Nia na Bi. Sikitu. Isitoshe, serikali inachukua jukumu la kuwalinda vijana kutokana na dawa za kulevya pale Inspekta wa polisi anamshika Bw. Mambo ambaye ni mlanguzi wa dawa za kulevya.

Vilevile, imebainika kwamba wazazi wanachangia pakubwa katika kuendeleza changamoto zinazowakumba vijana. Ikiwa wazazi watatekeleza majukumu yao ipasavyo, vijana watapata msingi unaofaa kuweza kujitegemea maishani. Serikali pia inafaa kuyapa masuala yanayohusiana na vijana kipao mbele kwa sababu kizazi cha vijana kinalipa taifa lolote lile matumaini. Ni vyema pia serikali kuchukua hatua kukomesha dhuluma zinazotendewa vijana kupitia asasi mbalimbali kama vile elimu na siasa na kuwatambua vijana kama sehemu muhimu ya jamii. Vijana wanafaa kuwajibika katika majukumu yao ili maamuzi yao yaweze kuheshimiwa na wanajamii. Vijana wakikosa matumaini taifa litakosa msingi wa siku zijazo. Ni muhimu pia serikali kuweka sera mwafaka kuhusu elimu na ajira ya vijana pamoja na kuzingatia ufaafu wa sera hizi kwa vijana kwa kuwa kuimarika kwa maisha ya vijana ni kuimarika kwa taifa.

## MAPENDEKEZO

Utafiti huu umejibana kwenye changamoto zinazowakumba vijana. Mtafiti amependekeza tafiti za baadaye zichunguze mchango wa fani katika kushughulikia masuala ibuka na changamoto zinazowakumbwa wanajamii kwa ujumla. Hii ni kwa sababu pana mwingiliano mkubwa baina ya fani na masuala mengine yanayoelezwa na waandishi. Pia, Mtafiti angependekeza utafiti wa baadaye uchunguze changamoto zinazowakumba vijana katika tanzu zingine za fasihi kama vile ushairi na hadithi fupi.

## MAREJELEO

Chepkwony, A. (2005). *The Youth*: A challenge to the Church in Africa Today.

Flaubert, G. (1850). *Realism Theory in the Making: A Ideological Perspective*. London. Merlin Press.

Hegel, G. (1979). *Introduction to Aesthetics*. Oxford: Clarendon.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (2007). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Vide Muwa Publishers Limited.

Lukacs, G. (1963). *The meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press. Mbatiah, M. (2005) *Upotevu* . Nairobi: Phoenix Publisher Limited.

Mohamed, S. (2000) *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Limited.

Momanyi, C. (2006) *Tumaini*: Vide Muwa.

Mutua, J. (2007). Mitazamo ya Vijana na Wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Nairobi (tasnifu ambayo haijachapishwa).

Naliaka, R. (2012). Uhakiki wa hali ya vijana katika Riwaya ya Vipanya vya Maabara. Chuo Kikuu Cha Nairobi (tasnifu ambayo haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimera R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Natharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Obure, E. (2012). Dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya za Rosa Mistika na Tumaini. Chuo Kikuu Cha Nairobi (tasnifu ya M.A).

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.